

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**WASTAAFU MKOA WA DAR ES SALAAM WAIOMBA SERIKALI KUPUNGUZA TOFAUTI
YA PENSHENI.**

Maelfu ya wastaafu Mkoa wa Dar es salaam wanaolipwa na Wizara ya Fedha na Mipango, wamejitokeza kwa wingi kuhakikiwa huku wakiiomba Serikali kujitahidi kuweka uwiano wa pensheni kati ya wastaafu wapya na wale wa miaka ya nyuma.

Wakizunguza katika Ukumbi wa Karimjee uliopo jijini Dar es salaam, wastaafu hao wamepongeza utaratibu wa sasa katika kuwahakiki kwa kuwa unafanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia uhitaji wa wale wenye mahitaji maalum, wakiwemo wasiojiweza na wagonjwa katika kupatiwa huduma.

Baadhi ya wastaafu hao wameiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa utofauti wa pensheni kati ya wastaafu wapya na wale wa zamani kwa kuwa bado kuna utofauti mkubwa ilihali thamani ya Shilingi kwa miaka ya nyuma na hali ya maisha kwa sasa yamebadilika sana.

Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Bw. Mohammed Mtonga, amesema kuwa Wizara ya Fedha na Mipango inaendesha zoezi la kuhakiki wastaafu wanaolipwa pensheni na wizara hiyo ili kuhuisha taarifa za wastaafu kwa lengo la kupata kanzidata (database) ili kuiwezesha Serikali kuwalipa wastaafu wanaostahili.

Amesema kuwa wastaafu wanaolipwa na Wizara hiyo ambao hawatahakikiwa wataondolewa kwenye orodha ya malipo ya pensheni kwa kuwa watakuwa wamekosa sifa. Hivyo amewaomba wastaafu hao popote walipo waitikie wito huo wa kufika maeneo ya kuhakikia ili kuondoa usumbufu hapo baadae.

Aidha Bw. Mtonga amewasisitiza wasaidizi wa wastaafu wasiojiweza kabisa wasisumbuliwe kuwaleta katika vituo vya uhakiki na badala yake walete nyaraka muhimu ambazo baada ya kupitiwa na kuchunguzwa, kutakuwa na

utaratibu maalumu wa kuwafuata huko walipo hata kama ni hospitalini, ili kuwapunguzia adha ambazo wangekumbana nazo wakati wa zoezi hilo.

Amewataka Wastaafu hao kufika wenyewe na sio kutuma wawakilishi ikiwa hawana matatizo makubwa ya kiafya, wakiwa na nyaraka zote muhimu zikiwemo barua ya tuzo ya kustaafu, barua ya kustaafu au kupunguzwa kazini, nakala ya hati ya malipo ya kiinua mgongo au mkupuo, barua ya ajira ya kwanza, kitambulisho cha pensheni, barua ya kuthibitishwa kazini, kadi ya Benki na picha mbili ndogo zilizopigwa hivi karibuni.

“Zoezi la kuhakiki wastaafu Mkoa wa Dar es salaam linalofanyika katika Ukumbi wa Karimjee na viwanja vya Mwalimu Nyerere (sabasaba), lililoanza Machi 6 na kutarajiwa kumalizika Machi 10, mwaka huu 2017, ndio linahitimisha zoezi la uhakiki kwa nchi nzima na baada ya hapo itajulikana kama kunamalipo yaliyokuwa yanalipwa isivyostahili ili kufanya marekebisho na kuchukua hatua stahili kwa mujibu wa sheria”. Alifafanua Bw. Mtonga.

Zoezi hilo la uhakiki linaloendelea Mkoa wa Dr es salaam, lilianza Oktoba 20, 2016 katika mkoa wa Pwani na limeshafanyika katika mikoa 25 ya Tanzania Bara ambayo ni Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Songwe, Katavi, Rukwa, Morogoro, Dodoma, Singida, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu, Geita, Kigoma na Tabora, Lindi na Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba-Zanzibar.

Imetolewa na:

B. Mwaipaja
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha na Mipango.